## Namna Ya Kulipia Matangazo Facebook na Instagram

Kulipia matangazo Facebook na Instagram ni rahisi sana kiasi kwamba kila mtu anaweza kufanya akiwa na simu yake mkononi tu

Sio lazima uwe na dollars Cash au US dollar account ili uweze kulipia matangazo...

***HAPANA!***

Hapa Tanzania kuna njia nyingi japo Mimi nashauri utumie njia mbili ambazo ni Nzuri na rahisi Kulipia yaani :

- Mpesa App
- Bank Transfer.

Kama uko nje ya Tanzania, huwa wana njia zao kila nchi zinazokupa urahisi na ufanisi zaidi...

Mfano

- Ghana wanatumia USD Card Kulipia
- Cameroon Wanatumia USD Card Kulipia
- South Africa Wanatumia Pay pal Kulipia.


## Sababu Zinazopelekea Tangazo lako Lishindwe Kukuletea Mauzo ×10 Zaidi Kwa Kutumia Facebook na Instagram Meta ads.

Nilipoanza Serious Kurusha matangazo Facebook mwenyewe bila kusaidiwa na Mtu mwingine, Niliweka budget ya **$20** Sawa na **50,000 Tsh** Kwa Wakati huo nilikuwa nauza huduma ya afya.

Na hii ilikuwa tarehe **20** mwezi **March 2023**

Na tangazo lilienda siku **Nne** tu

Tazama Hii Screenshot hapa Chini Niliamua Kuitunza Najua Ipo siku Nitakusimulia....




Baada ya kutumia hiyo budget unaweza kisia nini kilitokea...

ha! ha! ha! Siyo hivyo unavyofikiria

ILA...

Niliambulia Engagement na Kupigiwa Simu Nyingi za Watafuta taarifa bila kuuza chochote.

Ebu Fikiria Ndani huna kitu,

Na unaamua kuitumia PESA ambayo Ungeitumia kwenye mambo mengine ukaamua kuitumia kurusha matangazo ukiwa na matumaini Uuze Zaidi na mwisho wa siku unaambulia Patupu.

Na hii ndiyo hutokea Unapojaribu kuzalisha pesa bila kuwekeza kwenye ujuzi kwanza unaishia kupoteza tu.

***Na ndio kosa la kwanza Wafanyabiashara Tanzania wanalifanya Nikiwemo mimi wa kipindi kile!***

Hawana ujuzi, hawana mtu wa kuwaangoza na kuwaonesha kitu gani kinaleta matokeo na wafanye kitu gani.